

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI

11 MEI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 11 MEI, 2022

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**172. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni Vikundi vingapi vya Vijana wa Zanzibar vimenufaika na mikopo au uwekezaji kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Taifa.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **173. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kujenga vyumba vinne vya Madarasa na Bweni katika Shule ya Sekondari Matombo Kata ya Konde.

### **174. MHESHIMIWA JOHN MARKO SALLU (HANDENI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Kwasunga linalounganisha Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Bagamoyo.

### **175. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kusajili na kuboresha miundombinu ya Shule Shikizi zilizojengwa kwa nguvu za Wananchi.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **176. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme katika Kata mbili ambazo hazijawahi kupata umeme katika Jimbo la Ndanda.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **177. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMÈTE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la ukosefu wa maji katika Wilaya za Mkoa wa Mara.

### **178. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Shule zote nchini zinapata maji safi na salama.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA  
TAIFA:**

**179. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO  
(B.L.W):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali ina mpango gani na eneo lililoachwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika Shehia ya Kengeje – Pemba.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**180. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA  
(TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Tumbatu.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**181. MHESHIMIWA MUSSA OMAR SALIM  
(GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, kuna Mwongozo unaosema kuwa Zanzibar Insurance Corporation haipaswi kushiriki kukata Bima za Miradi mikubwa.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



*(Majadiliano yanaendelea)*

**11 MEI, 2022  
DODOMA**

**N.J. MWIHAMBI, ndc  
KATIBU WA BUNGE**